## Je! Ni kinyume cha sheria kutumia au kuwa na dawa za kulevya kwa matumizi yangu binafsi?

Nchini Kanada, **ni kosa kuwa na "dutu zinazodhibitiwa" kama dawa za kutia usingizi, kokeini, metamfetamini, na dawa changamshi za kuleta njozi, hata kwa matumizi yako binafsi ("umiliki rahisi")** isipokuwa kama umeandikiwa na daktari.

Sheria ya shirikisho inayodhibiti dawa hizi inaitwa *Sheria ya Dawa na Dutu Zinazodhibitiwa* (CDSA), na umiliki rahisi hauruhusiwi chini ya kifungu cha 4.

## Vipi kama nikiwa nimeandikiwa na daktari?

Ni halali kumiliki dawa ambayo umeandikiwa na daktari, ili mradi tu karatasi ya dawa iwe kwa jina lako. Kwa baadhi ya madawa, karatasi ya dawa pia ni lazima ikuidhinishe kuzibeba nje ya nyumba yako. Ni wazo zuri kuwa na karatasi yako ya dawa ikiwa unakusudia kubeba dozi zako. Ni kinyume cha sheria kumiliki dawa aliyoandikiwa mtu mwingine na daktari, hata kama amekupa. Ni kinyume cha sheria kumpa mtu mwingine dawa uliyoandikiwa wewe na daktari.

## Je! Kiasi cha dawa nilicho nacho kinaleta mabadiliko?

Ni kosa kubwa la jinai kumiliki dawa za kulevya kwa kusudi la kumpa mtu mwingine, iwe unaziuza au unazitoa bure (yaani "usafirishaji wa dawa za kulevya"). Katika sheria ya Kanada, hakuna "kiasi cha juu" maalum ambacho kinatofautisha kati ya kumiliki kwa ajili ya matumizi binafsi na kumiliki kwa ajili ya "usafirishaji."

Hata hivyo, polisi na mahakama zitazingatia kiasi cha dawa wakati wa kuamua kama mtu alikuwa na dawa za kulevya kwa ajili ya matumizi binafsi au kwa ajili ya usafirishaji (m.f. kadiri kiwango kinavyokuwa kikubwa, ndivyo huongezeka uwezekano wa kufikiriwa umemiiliki kwa ajili ya usafirishaji). Pia huzingatia vipengele kama vile kiasi cha pesa alizonazo mtu, na kuwepo wa vitu kama vile mizani na mifuko.

Pia kuna sheria tofauti kuhusu bangi inayoitwa *Sheria ya Bangi.* Ingawa matumizi ya bangi kwa burudani yalihalalishwa mnamo 2018, bado kuna vizuizi vya kumiliki dawa hiyo. Watu wenye umri wa miaka 18 na zaidi wanaruhusiwa tu kumiliki bangi ambayo wamepata kutoka kwa wauzaji walioidhinishwa na serikali au kuotesha hadi mimea minne ya bangi kwa kila kaya, na hadi gramu 30 tu za bangi iliyokaushwa katika sehemu ya umma.

Majimbo mingine pia yameweka sheria kuhusu kiwango cha juu cha bangi unachoweza kumiliki nyumbani.

Kila jimbo pia limeweka umri wa chini wa kumiliki bangi kwa ajili ya burudani.

Watu wanaweza kukabiliwa na mashtaka ya jinai kwa kumiliki bangi yoyote iliyopatikana *kinyume cha sheria* (yaani zisizopitia sehemu zilizoidhinishwa na serikali).

## HUKUMU NA ATHARI ZA TATHMINI ZA ASILI NA UTAMADUNI

Ubaguzi dhidi ya watu Weusi umeandikwa sana katika mfumo wa kisheria wa uhalifu nchini Kanada na mara nyingi husababisha hukumu kali (adhabu) kwa Watu Weusi. Tathmini ya Athari za Asili na Utamaduni (IRCAs) ni ripoti ambazo hutolewa na mwanasheria wako na kutumiwa na mahakimu wanapotoa maamuzi ya hukumu baada ya Mtu Mweusi au aliyebaguliwa kwa rangi kuhukumiwa kwa uhalifu. IRCAs zimeundwa ili kuwasaidia mahakimu kuelewa jinsi mambo kama vile ubaguzi wa rangi na umaskini yanavyochangia jinsi mtu Mweusi au mtu aliyebaguliwa kwa rangi kuhukumiwa kwa uhalifu. IRCAs zinaweza kupendekeza uamuzi tofauti na kufungwa jela, au hukumu ya jela inayozingatia utamaduni wa mtu

Ikiwa unashutumiwa kwa uhalifu na unajitambulisha kama mtu Mweusi, unapaswa kuzungumza na wakili haraka iwezekanavyo kuhusu ripoti ya IRCA na ushirikiane naye ili kupata ripoti madhubuti ya IRCA.

Kwa taarifa kuhusu haki zako wakati polisi wanapokusimamisha kuhusu kosa linalohusu madawa ya kulevya angalia tovuti yetu ya **www.hivlegalnetwork.ca/ACB-KYR**

TUNATAMBUA MSAADA WA KIFEDHA WA:

Department of Justice Canada | Ministère de la Justice Canada

**KIJITABU HIKI NI CHA SASA HADI AGOSTI 2024, LAKINI SHERIA INAWEZA KUBADILIKA.**

# FAHAMU HAKI ZAKO

## katika sheria za dawa za kulevya kwa watu wa Afrika, Karibiani, na Weusi (AKW) wanaotumia dawa za kulevya





**Ocean Meets Sky** (Jeff Duke)

# KOTE KANADA,

## WATU WA AFRIKA, KARIBIA NA WEUSI (AKW) WANAKABILIWA NA GHASIA ZINAZOIDHINISHWA NA SERIKALI AMBAZO ZIMEKITA MIZIZI KATIKA URITHI WA UTUMWA NA KUWEPO KWA UBAGUZI WA RANGI WA KUDUMU DHIDI YA WATU WEUSI, AMBAO UNADHIHIRIKA KATIKA SHERIA ZA DAWA ZA KULEVYA ZA KANADA.

Kijitabu hiki kinajibu maswali kuhusu sheria za dawa za kulevya za nchini Kanada ili kutoa ufahamizi bora wa makosa ya dawa za kulevya pamoja na mamlaka ya polisi, waendesha mashtaka, na mahakama.

**Kinatoa taarifa za kisheria, si ushauri wa kisheria.** Taarifa za kisheria zinaweza kukusaidia kuelewa sheria, lakini ni za jumla. Ushauri wa kisheria ndio muhimu husuan na hali yako. Ikiwa unataka au unahitaji ushauri wa kisheria, unapaswa kuzungumza na mwanasheria. (Tazama www.hivlegalnetwork.ca/BlackCommunities kwa taarifa kuhusu namnai ya kupata mwanasheria.)

Uvunjaji wa sheria yoyote kati ya hizi unaweza kusababisha kifungo cha hadi miaka mitano kwa wale walio na umri wa miaka 18 na zaidi na kifungo cha vijana kwa wale walio chini ya miaka 18. Majimbo binafsi yanaweza kuwa na sheria za ziada zinozisimzmia iwapo matumizi huweza kufanyika au la.

### VIGHAIRI VINGINE VINAVYOWEZA KUSABABISHA KOTOFUATWA KWA KANUNI ZA MASHTAKA YA UMILIKI RAHISI WA DAWA CHINI YA CDSA:

**Ikiwa uko katika mazingira ya kuzidisha dozi:**

- Sheria ya ***Msamaria Mwema ya Kuzidisha Dozi ya Dawa*** inaweza kuzuia polisi kukutoza wewe na wengine katika mazingira ya kuzidisha dozi, ikiwa umetafuta usaidizi wa matibabu kwa ajili yako au kwa mtu mwingine ambaye amezidisha dozi. Katika hali hii, polisi hawawezi kukushtaki kwa umiliki rahisi, au kwa kukiuka masharti yoyote ya msamaha wako, dhamana, muda wa majaribio, au hukumu ya masharti ("kizuizi cha nyumbani") inayohusiana na shitaka la umiliki rahisi lililopita
- Sheria ya *Msamaria Mwema ya Kuzidisha Dozi ya Dawa za Kulevya* haizuii polisi kukushtaki wewe na wengine kwa makosa mengine nje ya umiliki rahisi; hati za kukamatwa ambazo hazijakamilika; au kukiuka masharti yoyote ya msamaha wako, dhamana, muda wa majaribio, au hukumu ya masharti inayohusiana na kosa ambalo si la umiliki rahisi.

**Kama unaishi B.C, sheria mbalimbali hutumika. Angalia tovuti yetu kwa taarifa zaidi.**

### Je! Ninaweza kukamatwa kwa kutumia huduma za programu ya sindano na bomba la sindano, tovuti ya matumizi inayosimamiwa, au huduma ya kuzuia kuzidisha dozi?

Huwezi kukamatwa kwa kuwa tu kwenye programu ya sindano na bomba la sindano, tovuti ya matumizi inayosimamiwa, au kuwa katika kituo cha huduma ya kuzuia kuzidisha dozi.

Ingawa ni kinyume cha sheria kumiliki dawa fulani nchini Kanada (isipokuwa zilizoainishwa katika swali # 1 hapo juu), serikali inaweza kuwaachia wateja na waendeshaji wa tovuti ya matumizi inayosimamiwa au huduma ya kuzuia kuzidisha dozi, dhidi ya kufunguliwa mashtaka ya jinai kwa kupatikana na dawa haramu wakati wakiwa kwenye majengo.

Kimsingi, hii ina maana kwamba unaweza kumiliki na kutumia dawa za kulevya bila tishio la kufunguliwa mashtaka ya jinai, **ikiwa utafanya hivyo ndani ya kituo au huduma iliyoruhusiwa.**Hujasamehewa ukiwa katika usafiri kwenda kwenye kituo.

Mazingira mengine ya kupunguza madhara, kama vile programu ya sindano na bomba la sindano, hayajaondolewa kwenye sheria za dawa za Kanada, kwa hivyo bado unaweza kujiweka kwenye hatari ya mashtaka ya jinai ikiwa unatumia dawa ndani ya maeneo hayo (isipokuwa yaliyobainishwa katika swali # 1 hapo juu).

### Je! Ninaweza kushtakiwa kwa kuwa na vifaa vya kutumia dawa za kulevya?

Nje ya mazingira ya kupunguza madhara, huwezi kushtakiwa kwa jinai kwa *kuwa tu na* vifaa vya kutumia dawa za kulevya.

Hatujui mtu yeyote aliyewahi kushtakiwa kwa kuwa tu na vifaa vya kutumia dawa za kulevya ambavyo havijatumika.

Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba baadhi ya miji ina sheria maalum zinazokataza matumizi au "uonyeshaji" wa vifaa vya matumizi ya dawa za kulevya au "vifaa vya dawa za kulevya" katika maeneo ya umma.

### Vipi kuhusu kuwa na vifaa vya dawa vilivyotumika?

Kumiliki vifaa ambavyo vimetumika na vina chembechembe za dawa haramu za kulevya ni kinyume cha sheria kitaalamu, kama vile tu kumiliki dawa zenyewe ilivyo ni kinyume cha sheria.

Polisi wametaifisha au kuharibu vifaa vya matumizi ya dawa za kulevya walivyovikuta kwa watu na kutishia kuwakamata watu kwa sababu ya mabaki ya dawa za kulevya kwenye vifaa vyao. Au kwa njia nyingine, huweza kutumia vifaa vilivyotumika kama msingi wa kutafuta na kufungua mashtaka mengine.

Ingawa matukio kama haya yanaweza kuwa si ya kawaida sana, ni muhimu kufahamu kuwa *unaweza* kuwa katika hatari ya kufunguliwa mashtaka kwa kosa la kumiliki dawa haramu za kulevya (au makosa mengine, kulingana na matokeo ya upekuzi) kwa kumiliki tu vifaa baada ya kutumika.

